## Storybooks Canada

storybookscanada.ca

# Kwanini Viboko Hawana Nywele

Written by: Basilio Gimo, David Ker
Illustrated by: Carol Liddiment
Translated by: Matteo E. Mwita

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 3.0 International License.
https://creativecommons.org/licenses/by/3.0

# Kwanini Viboko Hawana Nywele

Basilio Gimo, David Ker
Carol Liddiment
Matteo E. Mwita
Kiswahili
Level 2

(imageless edition)

Siku moja, Sungura alikuwa akitembea pembeni ya mto.

Kiboko alikuwepo pia, akitembea huku akila majani mazuri ya kijani.

Kiboko hakumwona Sungura na kwa bahati mbaya akaukanyaga mguu wa Sungura. Sungura akaanza kumpigia Kiboko kelele. “We Kiboko huoni kama umeukanyaga mguu wangu?”



Sungura alikuwa na furaha kwa kuwa nywele za Kiboko ziliungua. Hadi leo kwa kuogopa moto, Kiboko hawezi kwenda mbali na maji.

Kiboko akaanza kulia na kukimbilia kwenye maji. Nywele zake zote zilikuwa zimeungua na moto. Kiboko aliendelea kulia, “Nywele zangu zimeungua na moto! Nywele zangu zote zimeisha! Nywele zangu nzuri!”



Kiboko akamwomba Sungura msamaha, “Samahani, sikukuona, tafadhali nisamehe!” Lakini Sungura hakukubali na akaendelea kumbwatukia Kiboko, “Umefanya makusudi! Kuna siku utakiona, na nitakulipizia!”

Sungura aliendakutafuta moto na akamwambia, “Nenda, ukamchome Kiboko akitoka majini kuja kula majani. Alinikanyaga!” Moto ukajibu, “Hakuna tatizo, rafiki yangu Sungura, nitafanya ulichoniomba kufanya.”



Baadaye, Kiboko alikuwa akila majani mbali na mto, aliposhtuka moto umelipuka. Miale ya moto ikaanza kuzichoma nywele za Kiboko.